



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA**



**TAARIFA KWA UMMA**

**Yah: WATAHINIWA WANAOTARAJIWA KUFANYA MTIHANI WA  
MARUDIO WA USAJILI NA LESENI TAREHE 16.2.2024**

**Dodoma, Tanzania**

**20.01.2024**

Ofisi ya Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania, inawatangazia watahiniwa wote wa ngazi ya Stashahada waliofutiwa matokeo ya mtihani wa Usajili na leseni uliofanyika tarehe **07.09.2023** kuwa mtihani huo utarudiwa tarehe **16.02.2024**.

Watahiniwa wote wanajulishwa kujisajili kwenye fomu iliyopo katika tovuti ya Baraza kwa ajili ya kuweka taratibu za maandalizi ya mtihani huu ikiwemo kutoa namba za mtihani. Zoezi hili litaanza tarehe **20.01.2024** hadi tarehe **12.02.2024** saa sita usiku.

Watahiniwa wote mtatakiwa kufika Kituo cha **Chuo Kikuu cha Mt. Yohana (St. John)-Dodoma** siku ya tarehe **16.02.2024** kuanzia **04:00 kamili** asubuhi mkiwa mmevaa Mavazi nadhifu kwa Mujibu wa Mwongozo wa Mavazi kwa Watumishi wa Umma. Pia, mtatakiwa kuja na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya Mtihani; Picha moja (**Passport size**) yenye viwango vilivyoelekezwa, Kalamu nyeusi au Penseli aina ya HB, Ufutio na Kitambulisho.

Aidha, Watahiniwa mnajulishwa kuwa Mtihani huu hauna Malipo. Ninawatakia maandalizi mema.

*Amama*

**Agnes Mtawa  
MSAJILI - TNMC**